50 Hadithi

# KUTAYAMMAM

Kutoka kwa Ammar bin Yasir, Mungu amuwiye radhi, amesema:

1 Mtume wa Mwenyezi Mtume (Rehema na amani ziwe juu yake) alinituma katika jukumu fulani, nikapatwa na janaba, lakini sikupata maji, nikajibiringisha katika mchanga kama mnyama, kisha nikaenda kwa Mtume (Rehema na amani ziwe juu yake) nikamsimulia tukio hilo.

2 Akasema: "hakika ilikuwa inatosha kufanya kwa mikono yako hivi" kisha akapiga ardhi kwa mikono yake mpigo mmoja, kisha akapangusa mkono wa kulia kwa mkono wa kushoto, na mkono wa kushoto kwa mkono wa kulia, na nje ya viganja vyake, na uso wake.[1]

1 Imepokewa na Al-Bukhari (347) na Muslim (368), na maneno ni kwa Muslim.

## Ayah

Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu

﴿Enyi mlioamini! Mnapo simama kwa ajili ya Sala basi osheni nyuso zenu, na mikono yenu mpaka vifundoni, na mpake vichwa vyenu, na osheni miguu yenu mpaka vifundoni. Na mkiwa na janaba basi ogeni. Na mkiwa wagonjwa au mmo safarini, au mmoja wenu ametoka chooni au mmewagusa wanawake, na hamkupata maji, basi tayamamuni vumbi lilio safi, na mpake nyuso zenu na mikono yenu. Hapendi Mwenyezi Mungu kukutieni katika taabu; bali anataka kukutakaseni na kutimiza neema yake juu yenu ili mpate kushukuru.﴾ [al maida: 6]

## Msimulizi

Anaitwa: Abu al-Yaqzan Ammar bin Yasir bin Amir al-Ansi al-Makki al-Badri, bosi wa Banu Makhzoum. Yeye na baba yake na mama yake walikuwa miongoni mwa wale walioteswa na makafiri wa Quraish kwa sababu ya kusilimu kwao. Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, alikuwa akiwapita na kusema: kuweni na subira enyi watu wa Yassir kwani hakika Ahadi yenu ni Pepo." Na mama yake ni Sumayyah, ambaye alichomwa na Abu Jahl kwa mkuki wake kwenye utupu wake hilo, na mwanamke huyo ndiye shahidi wa kwanza katika Uislamu.

Kwa sababu ya Ammar bin Yaasir Mwenyezi Mungu Mtukufu, aliteremsha Aya hii: {Isipokuwa yule aliyelazimishwa na hali moyo wake umetulia kwa imani} [An-Nahl: 106].

kuna khitilafu juu ya kuhama kwake kwenda Uhabeshi, na alihama kwenda katika mji wa Madina, na alihudhuria vita vyote, kisha akahudhuria vita ya yamaamah na sikio lake likakatwa katika vita hiyo, kisha Omar, Mwenyezi Mungu amuwie radhi, alimtumia kuwa kiongozi katika mji wa Kuufah., na akawaandikia watu wa kuufah kuwa: hakika Yeye –Ammar- ni miongoni mwa maswahaba watukufu wa Muhammad, rehma na amani ziwe juu yake. Amaar aliuawa Akiwa na umri wa miaka thelathini na saba, na alizikwa huko kuufah. Na Mtume (saw.) aliwahi kumuambia kuwa: "Kundi la madhalimu litakuuwa"[1]

## Muhtasari

Ammar bin Yasir, Mwenyezi Mungu amuwie radhi yeye na wazazi wake, alipatwa na janaba katika baadhi ya safari zake na hakuweza kupata maji, hivyo akajizungusha kwenye udongo mpaka ili aweze kuswali. Aliporejea kwa Mtume (Rehma na amani ziwe juu yake) akamueleza Mtume akambainishia asili ya tayammam, na kwamba ni pigo moja katika udongo ambalo anapangusa nalo mikono na uso.

1 Rejea ufafanuzi wake katika: "Al-Tabaqat Al-Kubra" cha Ibn Saad (3/186), "Al-Isbah fi Tamyiiz Al-Sahaba" cha Ibn Hajar (7/291), "Tahdheeb Al-Kamal" cha Al- Muzzi (21/215), "Sir Al-Alam Al-Nubala" cha Al-Dhahabi (3/ 245).

# Ufahamu

Tayammum ni ruhusa iliyowekwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa waja wake pale wanapokosa maji au kushindwa kuyatumia ili kuwarahisishia, na Mtume, rehma na amani ziwe juu yake, alisema: “Mwenyezi Mungu anapenda kutumiwa ruhsa zake kama anavyochukia kuasiwa.”[1] na Wanachuoni wameifafanua kuwa tayammam ni: kukusudia mchanga - vumbi – ili kupangusa uso na mikono kwa nia ya kuhalalikiwa kuswali na mfano wa hayo[2]. Ni sheria iliyothibiti katika Qur’an, na Sunnah na makubaliano ya wanazuoni, na ni ruhusa maalumu ambayo Mwenyezi Mungu Mtukufu ameiweka katika umma huu”[3]

1 Ammar (ra), anasimulia kuwa Mtume, (Rehma na amani ziwe juu yake), alimtuma katika baadhi ya majukumu yake, kisha akajiotea na akapatwa na janaba, akazungusha mwili wake mzima katika mchanga safi ambao una vumbi mpaka mchanga ukaenea mwili mzima; Ili aweze kuhalalikiwa swala na kusoma Qur’an na mengine yanayofanana na hayo, kisha aliporejea kwa Mtume, rehma na amani ziwe juu yake, akamsimulia tukio zima Ili aweze kufahamu kama alifanya sawa au alikosea.

Ammar alifanya hivyo kwa sababu aliona kwamba mchanga/udongo hutumika badala ya maji, Hivyo basi Kama maji yanavyopaswa kuenea mwili mzima katika kuosha na kujitwaharisha, hivyohivyo ndivyo inakuwa katika tayammam kwa mtazamo wake na jitihada zake.

2 Mtume (Rehma na amani ziwe juu yake) alimwambia kwamba ilikuwa inatosha kupiga ardhi kwa mikono yake mara moja, kisha kupangusa mikono na uso wake, kwa kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu aliposema: “Na mkiwa wagonjwa au mmo safarini, au mmoja wenu ametoka chooni au mmewagusa wanawake, na hamkupata maji, basi tayamamuni vumbi lilio safi, na mpake nyuso zenu na mikono yenu”.



1 Imepokewa na Ahmad (5866).
2 “Nail al-Awtar” cha al-Shawkani (1/319).
3 “Nail al-Awtar” cha al-Shawkani (1/319).

# Mafunzo

1. Kitendo cha Ammar Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake kinaashiria kwamba ni wajibu kwa Muislamu asipofahamu hukumu mojawapo ya masuala fulani, ambayo hajui hukumu yake wala kauli ya wanazuoni katika hilo, na muda wa kumuuliza mtu mwingine ukawa hautoshi au yuko safarini na asiweze kupata fat-wa; basi wakati huo inabidi kujitahidi kadiri awezavyo, kisha ikiwa atampata wa kumuuliza, ili kujua hukumu sahihi ya kisheria juu ya suala hilo basi afanye hivyo.

2. Katika hadithi hii inaashiria kuwa mwenye kujitahidi na kufasiri maana, ikiwa atakuwa miongoni mwa watu waliokidhi vigezo vya ijtihadi na akafasiri maana ya masuala Fulani, akawa amepatia sehemu na kukosea sehemu nyingine, basi si lazima kurudia kitendo hicho, kwani Mtume (Rehma na amani ziwe juu yake) hakumuamuru Ammar arudie; Kwa sababu alikosea katika sheria lakini alijitahidi, lakini alifanya twahara kwa namna isiyozingatiwa.[1]

3. Hadithi hii inaashiria kuwa sheria ya Uislamu ina kheri nyingi na wepesi, kwani haimtwiki mtu asiyoweza kufanya, ndio maana ikaruhusu tayammam, na kuridhika na kupangusa mikono na uso.



1 “’Iikmal Almuealim Bifawayid Muslimin”cha Qadi Iyadh (2/223).

